**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI MARIRE.
S.L.P 8105,
MOSHI.
15/12/2021
**SIMU 075444056**

Kumb. Na.Mrss/JI/2021/vol 01

Jina la Mwanafunzi ..........................................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDAR MARIRE WILAYA YA HAI, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021**

**1.0 Utangulizi**

Nina furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Marire mwaka 2021.

Muhula wa kwanza unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kwanzia tarehe tajwa bila kukosa.

**2.0 Mahitaji muhimu ya shule**

a) SARE YA SHULE

**Wavulana:** Shati mbili nyeupe na suruali mbili za rangi ya **Dark bluu (Kitambaa kimeambatanishwa) upana wa suruali uwe inchi 7.** Rangi ya sweta ifanane na rangi ya suruali. Viatu pea mbili nyeusi vya ngozi vyenye kamba, visiwe raba na visiwe na kisigino na soksi pea mbili rangi nyeusi. Tisheti ya rangi nyekundu.

**Wasichana:** Blauzi mbili nyeupe na sketi mbili rangi **Dark blue (Kitambaa kimeambatanishwa) sketi iwe pana na urefu upite kifundo cha mguu (yaani sketi iwe ndefu mpaka chini)**, juu ya hapo mwanafunzi hatapokelewa. Rangi ya sweta la shule ifanane na rangi ya sketi, viatu pea mbili vya ngozi vyenye kamba, visiwe raba na visiwe na kisigino na soksi pea mbili rangi nyeupe. Tisheti ya rangi nyekundu.

Jezi ya michezo kwa shule hii ni jezi za rangi bluu kwa wavulana na wasichana.

Tafadhali mzazi zingatia rangi ya kitambaa (kilichoambatanishwa hapo juu) ili kuepuka usumbufu kwa mzazi, mwanafunzi na shule.

b) **VIFAA VYA TAALUMA**

Daftari tisa za Quire 3 na daftari ndogo tisa za mazoezi, kalamu za bluu, mkebe wa hesabu (compass), rula, penseli na ufutio. Begi imara la kubebea vifaa vya shule.

c) **Mwanafunzi afanyiwe vipimo katika hospitali ya serikali kwa kujaziwa MEDICAL EXAMINATION FORM (imeambatanishwa)**

d) **Fomu zote zilizoambatanishwa zijazwe kwa usahihi na zirudishwe shuleni siku ya kuripoti.**

**KUTAKUWA NA KIKAO CHA WAZAZI WOTE WA WANAFUZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA MARIRE SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 TAREHE 07/12/2020 SIKU YA JUMATANO SAA TATU KAMILI ASUBUHI (03:00) BILA KUKOSA**

**KARIBU SANA MARIRE SEKONDARI**

..............................................

**N.E.KAGONJI**
**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
MARIRE SEC. SCHOOL
P. O. Box 8105
MOSHI

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo y Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu nchini. Mambo yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa na wanafunzi wote:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, jamii nzima na wanafunzi wenzako;

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni nyumbani;

d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kwa ukamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

e) Kuzingatia usafi wa mwili wako, mavazi na mazingira ya shule kwa ujumla;

f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

h) Kutunza mali za umma, mali za wengine na mali zako binafsi.

### 3.2 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule

a)Wizi

b)Uasherati na ushoga

c)Ubakaji

d)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.

e)Kupigana au kupiga.

f)Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g)Kudharau bendera ya Taifa.

h)Kuwa mjamzito/kupata mimba.

i)Kuoa au kuolewa

j)Kutoa mimba.

k)Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l)Kukataa adhabu kwa makusudi.

m)Kuwa na simu ya mkononi.

## SHULE YA SEKONDARI MARIRE

## AHADI YA KUKUBALI NAFASI NILIYOPATA

**A. Sehemu ya mwanafunzi:**

Mimi..........................................................................................................nakubali

Kupokea nafasi hii ya masomo katika shule ya sekondari Marire .Naahidi kuwa nitatii

Sheria zote za shule, nitakuwa mwaminifu, nitajitahidi kujifunza kwa bidii kwa kadiri ya uwezo wangu na kufanya kazi nyingine zote nitakazopangiwa kwa juhudi na maarifa.

Nitafika shuleni siku zote za masomo bila kuchelewa.

NB: Kushindwa kwangu kutii ahadi hii, kanuni na sheria za shule zichukue mkondo wake.

Saini ya Mwanafunzi...........................................

Anuani ya Nyumbani...........................................

...............................................

................................................

**B. Sehemu ya Mzazi/Mlezi ( AHADI)**

Mimi...........................................................nimekubali kumpatia mwanangu (Jina la Mwanafunzi husika)..................................mahitaji yote muhimu ya shule ( sare ya shule, vifaa vingine , madaftari nk) ili aweze kusoma na kujifunza bila matatizo. Naahidi pia kushirikiana na walimu katika kumlea na kumhudumia kadri ya uwezo wangu.

**SAINI YA MZAZI /MLEZI...................................................**

**ANWANI.........................................................................**

**.........................................................................**

**.........................................................................**

**SIMU..............................................................................**

PRESINDENT'S OFFICE- RALG

HAI DISTRICT COUNCIL

MARIRE SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(*This form should be filled by government officer*)

STUDENT FULL NAME……………………………………………………………………………..

AGE…………………………………

BLOOD COUNT (red and white)……………………………………………………………………

STOOL………………………………………………………………………………………………

URINE………………………………………………………………………………………………

V.D…………………………………………………………………………………………………

T.B…………………………………………………………………………………………………

EYES………………………………………………………………………………………………

EARS………………………………………………………………………………………………

TEETH………………………………………………………………………………………………

SKIN…………………………………………………………………………………………………

PREGNANCY………………………………………………………………………………………

TREATMENT GIVEN (if any)………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

ABDOMEN…………………………………………………………………………………………

HEART……………………………………………………………………………………………

ANY ADDITIONAL INFORMATIONS e. g Physical defect, infections, impairments and other abnormalities if required special care…………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

SIGNATURE…………………………………………

NAME………………………………………………

DATE………………………………………………

OFFICIAL STAMP…………………………………..